JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470
Nukushi: +255262963117
Barua pepe: **ps@mit.go.tz**
Tovuti: **www.mit.go.tz**

Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S. L. P 2996,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA MUHIMU NCHINI KWA MWEZI DESEMBA 2022

1. UTANGULIZI

Ndugu Waandishi wa Habari;

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kufanya tathmini ya mwenendo wa bei za bidhaa muhimu nchini kwa lengo la kutoa taarifa kwa Wananchi kuhusu mwenendo wa bei nchini. Taarifa hizi ni muhimu kwa ajili ya kuwawezesha wadau ikiwa ni pamoja na wazalishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali, walaji wa bidhaa hizo, wenye viwanda na wafanyabiashara kupata taarifa sahihi ili kufanya maamuzi sahihi yatakayochangia kukuza uchumi na kipato katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, kaya na Taifa kwa ujumla.

Ndugu Waandishi wa Habari;

Mwenendo wa bei za bidhaa umeendelea kuonesha tofauti za viwango vya bei za jumla na rejareja ambapo bei za baadhi ya bidhaa hasa za vyakula zimeongezeka kutokana na kupungua kwa uzalishaji kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022. Aidha, pamoja na upungufu katika uzalishaji kutokana na hali ya hewa isiyoridhisha kwenye maeneo mengi nchini na nchi jirani; mahitaji ya bidhaa za vyakula kwenye nchi jirani yameongezeka na hivyo kuongeza bei. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli duniani zinazochangia mfumuko wa bei umeendelea kuimarika na bei za bidhaa hizo zimeendelea kushuka na hivyo kupunguza gharama za uzalishaji, usafirishaji na uagizaji wa bidhaa na malighafi.zinazotumika katika uzalishaji kutoka nje ya nchi. Bidhaa za vyakula zilizoathirika zaidi na upungufu wa mvua na hivyo bei zake kupanda ni pamoja na maharage na viazi mviringo.

Ndugu Waandishi wa Habari;

Wizara inaendelea kuratibu ukusanyaji wa takwimu za bei za mazao kutoka kwenye masoko yaliyopo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kupitia Wakusanya Taarifa za Masoko (Market Monitors). Wizara pia inaratibu ukusanyaji wa taarifa za bei za bidhaa muhimu kama vile bidhaa za vyakula na vifaa vya ujenzi kupitia Maafisa Biashara wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imeendelea kukusanya taarifa za bei kutoka katika masoko yaliyopo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kukokotoa kiwango cha mfumuko wa bei kila mwezi. Kutokana na takwimu hizo. bei za bidhaa kwa

kila Mkoa hupatikana kwa kukokotoa wastani wa bei za mazao na bidhaa katika Mikoa hiyo.

2. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA ZA VYAKULA

i. Mahindi

Bei ya mahindi kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 750 na 1,890 kwa kilo. Bei ya chini na ya juu imepanda kutoka 700 na 1500 kwa kulinganisha na mwezi Novemba. Mikoa yenye bei ya juu ni Kilimanjaro, Mara na Kigoma na bei ya chini ipo katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Songwe na Ruvuma.

ii. Unga Mahindi

Bei ya Unga wa mahindi kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 1,200 na 2,050 kwa kilo. Bei ya chini ya unga wa mahindi imepanda kutoka 1,000 ukilinganisha na mwezi Novemba. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Iringa na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Mara, Kigoma na Kagera.

iii. Mchele

Bei ya mchele kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 2,200 na 3,500 kwa kilo. Bei ya chini na ya juu imepanda kutoka 2,000 na 3,200 kwa kulinganisha na mwezi Novemba. Mikoa yenye bei ya chini ni Katavi na Ruvuma na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kagera, Manyara na Arusha.

iv. Maharage

Bei ya maharage kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 2,200 hadi 3,650 kwa kilo. Bei ya chini imepungua kwa Shilingi 260 kwa kilo ikilinganishwa na mwezi Novemba. Bei ya juu imepanda hadi Shilingi 3,650 kutoka Shilingi 3,250 mwezi Novemba. Bei ya chini inapatikana katika Mkoa wa Katavi na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Manyara na Tabora.

v. Viazi Mviringo

Bei ya Viazi Mviringo kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 688 na 1,875 kwa kilo. Bei ya juu ya Viazi Mviringo imepanda kwa Shilingi 375 ikilinganishwa na mwezi Novemba. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Njombe, Songwe na Mbeya na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Mara na Dar es Salaam.

vi. Unga wa Ngano

Bei ya unga wa ngano kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 2,000 na 2,500 kwa kilo. Bei ya unga wa ngano imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na mwezi Novemba. Bei ya juu ipo katika Mikoa ya Manyara, Rukwa na Songwe na bei ya chini ipo katika maeneo mengi nchini.

vii. Sukari

Bei ya sukari kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 2,600 na 3,000 kwa kilo. Bei hiyo imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na mwezi Novemba. Hali hiyo inatokana na jitihada zinazoendelea za kuvutia uwekezaji na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa sukari nchini.

viii. Mafuta ya Kupikia

Bei ya mafuta ya kupikia ya Alizeti kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 4500 na 7,750 kwa lita. Vile vile, bei ya mafuta ya kupikia ya Mawese (Korie na Safi) kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 5,000 na 7,600 kwa lita. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya Alizeti ipo katika Mikoa ya Manyara, Iringa, Tabora na Dodoma na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Mtwara, Mara, Kigoma, na Ruvuma.

3. MWENENDO WA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI

i. Saruji

Bei ya saruji kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 15,000 na 24,000 kwa mfuko wa kilo 50. Bei hiyo imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na mwezi Novemba. Mikoa yenye bei ya chini ni Tanga, Dar es Salaam, Mtwara, na Pwani na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Kagera, Kigoma na Katavi.

ii. Nondo

Bei ya nondo mm 12 kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 22,650 na 28,000. Bei ya nondo mm 12 imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na mwezi Novemba. Bei za chini zipo katika Mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Salaam na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Katavi, Kagera, Iringa na Njombe.

Bei ya nondo mm 10 kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 18,000 na 22,500. Bei ya nondo mm 10 imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na mwezi Novemba. Bei za chini zipo katika Mikoa ya Iringa, Kilimanjaro na Mara na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Tabora, Kagera, na Songwe.

iii. Bati

Bei ya bati nyeupe geji 28 kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 30,500 na 38,000. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Iringa na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Manyara na Mara.

Bei ya bati nyeupe geji 30 kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 23,000 na 27,500. Bei ya juu ya bati imeshuka kutoka Shilingi 28,500 ukilinganisha na mwezi Novemba. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Shinyanga, Songwe, Njombe, Mbeya, Katavi Tanga na Dodoma na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Mara, Kilimanjaro, na Manyara.

4. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA NYINGINE

i. Hali ya uzalishaji wa bidhaa za Sabuni nchini

Ndugu Waandishi wa Habari:

Nchi yetu ina jumla ya viwanda vikubwa 8 vya sabuni (Detergent and Bar soaps) ambavyo vinahudumia soko la ndani na pia soko la nje hasa katika nchi za Uganda, Burundi, Malawi, Zambia na DRC. Aidha, kiasi kikubwa cha sabuni zinazotumika hapa nchini hutengenezwa na wajasiriamali wadogo waliopata mafunzo kutoka SIDO, VETA, na Taasisi Binafsi. Hata hivyo, kutokana na mahitaji ya sabuni kuwa makubwa kuliko uwezo uliopo wa uzalishaji wa ndani, sabuni zenye viwango tofauti vya ubora huagizwa kutoka nje, na hivyo kumwezesha mtumiaji wa mwisho kuwa na uchaguzi wa aina ya sabuni kulingana na mahitaji yake.

Ndugu Waandishi wa Habari:

Serikali kupitia Sera ya Maendeleo ya Viwanda inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Viwanda vinavyozalisha bidhaa za sabuni hususan sabuni za maji na sabuni za unga ikiwa ni pamoja na kurahisisha taratibu za uingizaji wa malighafi muhimu zinazotumika katika uzalishaji wa sabuni kutoka nje ya nchi.

ii. Mwenendo wa bei za Sabuni za Miche

Bei ya Sabuni aina ya Jamaa, White wash na MO kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 3,500 na 4,000. Bei ya chini ipo katika Mikoa mingi nchini na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Rukwa.

Bei ya Sabuni aina ya Takasa, Kiboko na Kuku kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 1,600 na 3,500. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Katavi, Dodoma, Geita na Morogoro na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Rukwa na Ruvuma.

Bei ya Sabuni aina ya Magadi kwa mwezi Desemba ni kati ya Shilingi 1,000 na 3,500. Sabuni za magadi zipo aina mbili nazo ni miche myembamba na miche minene. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Katavi, Kigoma, Mwanza, Mtwara na Tanga na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Njombe na Dodoma.

5. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA ZA VYAKULA KWA NCHI JIRANI

Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake kwenye kiasi cha mavuno ya mazao muhimu ya chakula kama mchele, mahindi, maharage na viazi mviringo; mahitaji ya bidhaa hizo kwenye nchi jirani yamekuwa makubwa kuliko uzalishaji, hivyo kuchangia kupanda kwa bei za bidhaa za vyakula nchini na nchi jirani.

Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki (TZS)

	Rwanda	Kenya	Uganda	Tanzania
Mafuta ya Kupikia	8,000	10,000	7,900	6,200
Maharage	2,300	3,045	3,000	2,925
Mahindi	1,500	1,880	1,850	1,275
Unga wa mahindi	2,200	2,538	2,500	1,625
Mchele	2,700	4,136	3,500	2,850

***Chanzo**: World Food Programme (WFP) na Global Product Prices*

Aidha, kwa ujumla bei za vyakula katika nchi nyingi duniani zimepanda ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2021. Mfumuko wa bei za vyakula hasa nafaka kama vile ngano umetokana na athari hasi za vita kati ya Urusi na Ukraine na majanga mengine kama vile UVIKO 19 na ukame ulioathiri uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2021/2022. Hata hivyo, mfumuko wa bei nchini Tanzania ni wa kiwango cha chini zaidi ikilinganishwa na nchi jirani ambapo Tanzania mfumuko wa bei kwa mwezi Novemba ni asilimia 4.9, Kenya asilimia 7.38, Uganda asilimia 10.6 na Rwanda asilimia 21.7.

6. UPATIKANAJI WA TAARIFA ZA MASOKO

Ndugu Waandishi wa Habari;

Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa taarifa za uhakika za bei za bidhaa na masoko, kufanya uchambuzi na kusambaza kwa wadau. Tutaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kupitia Idara mpya ya Uwekezaji Viwanda na Biashara iliyoanzishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini tupate taarifa za kuaminika kwa wakati kutoka maeneo yote nchini. Napenda kutumia fursa hii kuwahimiza Maafisa Biashara kote nchini kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu mwenendo wa bei kwenye maeneo wanayosimamia ikiwa ni pamoja na kukusanya taarifa za bei na kuziwasilisha kwa wakati Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

7. HITIMISHO

Ninapenda kuhitimisha taarifa yangu kwa kuuhakikishia umma wa Watanzania kuwa, Serikali inaendelea kufuatilia na kufanya tathmini ya bei za bidhaa muhimu ili kulinda maslahi ya wadau wote ikiwa ni pamoja na wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa husika. Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kuwahimiza Wafanyabiashara kote nchini kuendelea kuzingatia misingi ya ushindani wa haki katika kufanya biashara ili kuunga mkono jitihada za Serikali za kukuza uchumi kwa manufaa ya Wananchi wote. Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula ili kudhibiti mfumuko wa bei nchini.

Ndugu Waandishi wa Habari:

Tunapoelekea kwenye kipindi cha sherehe za mwisho wa mwaka, napenda kutoa rai kwa wafanyabiashara kote nchini kuepuka tabia ya upandishaji holela wa bei za bidhaa na kuzingatia maadili ya kibiashara na ufanyaji biashara wakati wote.

Napenda kuhitimisha taarifa hii kwa kuwatakia Watanzania wote Heri ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2023.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

.....

Exaud S. Kigahe (Mb.)

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

DESEMBA, 2022